**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA**

SHULE YA SEKONDARI MAZAE
S.L.B 131
MPWAPWA
**05/04/2023**

Simu ya Mkononi: **0784-49 05 85** – Mkuu
**0755-94 68 44** – Makamu
**0714-52 70 31** – Malezi

**KUMB.NA: MZE/ED/SS/JI/01/2023**

Kwa Mzazi wa……………………………………..
……………………………………………………………
……………………………………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MAZAE HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA MKOA WA DODOMA MWAKA 2023**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2023 tahasusi ya ………….. Shule ya sekondari **MAZAE** ipo **MPWAPWA** umbali wa kilometa **120 kutoka Dodoma mjini** Usafiri wa basi kutoka Dodoma mjini unapatikana katika kituo cha mabasi**- Soko la Ndugai** (Nane nane) na nauli ni **shilingi 7,000 hadi MPWAPWA.** na shukia kituo cha **MWANAKIANGA** kisha utapanda bodaboda hadi shuleni **TSH 1000/=**.kwa wale wanaotokea **DAR ES SAALAM NA MOROGORO** panda basi la moja kwa moja linalokuja MPWAPWA likitokea DSM au basi lolote linalopitia MBANDE wilaya ya KONGWA na shuka hapo, panda magari yanayo kuja **MPWAPWA** Shukia kituo cha (**Mwanakianga)** na utapanda bodaboda mpaka shuleni nauli **TSH 1,000/=** kwa wale wanaotokea **MOSHI,ARUSHA na MANYARA** kuna basi la moja kwa moja kutokea **ARUSHA** hadi **MPWAPWA** pia utashukia hapo hapo **mwanakianga**. Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **14/08/2023**.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia**

**2.1 Sare ya shule.**

a) Sare ya shule hii ni shati nyeupe la mikono mifupi na sketi ya rangi ya nyekundu marinda makubwa yasiyozidi nane, kitambaa kizito, iwe ndefu inayokaribia kiwiko cha mguu (Ankle).
b) Rangi ya hijabu ifanane na sare ya shule.
c) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
d) Soksi jozi mbili nyeupe.
e) Sweta rangi ya kijani ya jeshi (dark green)
f) Nguo za kushindia (**shamba dress**) ni sketi ya kijani yenye marinda ya kawaida ambayo itavaliwa na T-shirt ya shule pamoja na track suit yenye rangi ya blue na T- shirt ya blue ataivaa wakati wa michezo na wakati wa jioni.
g) Tai ndefu rangi nyekundu.

**2.2 . Michango ya shule**

a) Michango ya shule kwa mwaka ni shilingi **80,000.00** kwa mwanafunzi wa bweni. Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule NO. **50401200044 (Mazae Secondary School Revenue Collection).** katika benki ya **NMB**. (Tafadhari andika majina ya mwanafunzi kwenye pay in slip hata kama ni mtu mwingine anamlipia)

## Mchanganuo wa Fedha b) Michango inayotakiwa kulipwa na mzazi ni:-

| Na | Aina ya mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| 4 | Huduma ya kwanza | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/** |

**a) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-**

i. Ream 2 za karatasi kwa mwaka- Zitolewe zote mwanzo wa mwaka.
ii. Vitabu vya masomo tahasusi (orodha imeambatanishwa)
iii. Godoro la futi mbili na nusu kwa sita .
iv. Shuka mbili rangi ya bluu na rangi ya pink (lazima) yatatandikwa kwa utaratibu ambao utaukuta
v. Mto kwa ajili ya kulalia pamoja na chandarua.
vi. Sanduku (trunker) imara la kuhifadhia mali yake kwa usalama bwenini.
vii. Vyombo safi vya chakula ,sahani, bakuli, kikombe na kijiko.
viii. Ndoo mpya ya plastiki ya lita 10 yenye mfuniko kwa ajili ya kuhifadhia maji ya kuoga, kufulia na matumizi mengine binafsi.
ix. Galoni au chombo kidogo cha kuhifadhia maji ya kunywa.
x. Kwanja/fyekeo 1, jembe 1 reki 1, fagio la ndani 1, na ( **fagio la nje 1 kwa muhula**) na squeezer 1.
xi. Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biologia
xii. Scientific Calculator ( kwa wanafunzi wa sayansi).
xiii. Dawa ya kusafishia choo lita 5 aina ya **CARELINE**
xiv. Ili kurahisisha swala zima la malezi kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na T-SHIRT yenye nembo ya shule ambayo inapatikana hapa shuleni kwa kiwango cha Tsh. 15,000/=

**ANGALIZO**

* Mzazi unashauriwa kumpatia mwanao mahitaji ya kutosha kwani hataruhusiwa kutoka nje ya shule kwa muda wote wa masomo.

*-Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki **simu ya mkononi hapa shuleni**.Tafadhari sana ten sana na kwa heshima kubwa mzazi/mlezi mwenzetu **usimruhusu mtoto wako kuja na simu ya mkononi** kwa namna yeyote ile.Ikitokea amekuja nayo **ataadhibiwa kwa mujibu wa sheria za shule romani (M)**

*-Ili kurahisisha utumaji wa fedha kwa wanafunzi, mara mtoto afikapo hapa shuleni atashauriwa kufungua akaunti ya **NMB au CRDB** na mzazi utatuma fedha kupitia akaunti hizo kwa ajili ya matumizi ya mtoto.

### 3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

a. Wizi
b. Uasherati na ushoga
c. Ubakaji
d. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocane, mirungi, kubeli nk
e. Kupigana au kupiga, kutukana au kutukanana na mtu/mwanafunzi yeyote yule
f. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g. Kudharau Bendera ya Taifa au/na Wimbo wa Taifa na Wimbo wa Shule.
h. Kuoa au kuolewa au kuwekwa kimada
i. Kumpa mimba msichana,kupata mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule. j. Kutoa mimba
k. Kugoma,kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au/na watu
l. Kukataa adhabu kwa makusudi.
m. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi
n. kuwepo nje ya shule muda wowote ule wa shule bila kibali cha kumruhusu kutoka nje (kutoroka)

4. VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MPWAPWA DISTRICT COUNCIL**

**TO THE MEDICAL OFFICER**
**NAME OF STUDENT: …………………………………..……………………..AGE………….**
*MEDICAL HISTORY*

| | YES | NO |
|---|---|---|
| Tuberculosis | | |
| Asthma | | |
| Heart disease | | |
| Jaundice | | |
| Peptic ulcers | | |
| Epilepsy | | |
| Diabetes mellitus | | |
| Kidney problem | | |
| Anaemia | | |
| Neurosis | | |

**PHYSICAL EXAMINATION:**
Respiratory system - Cardiovascular system -
Gastrointestinal system -
Urinary system -
Reproductive system - Eye: R:-
L:-
E.N.T-

**INVESTIGATION**

1. Blood -HB……………………
-WBC………………….
-ESR……………………
-VDRL Test……………

2. Urine – Pregnancy……………………….. -Sed………………………………… -Stool……………………………….

I have examined the above student and considered that she is physically and mentally fit/ not physically and mentally fit for further studies.

Signature………………………………….. Designation;….………………………….

Station;…………………………………… Date;…………………………………….

## FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MAZAE

**FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI, KUKUBALI SHERIA ZA SHULE NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA**.

**A. TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI**:

1. JINA LA MWANAFUNZI: ……………………………………………………………………………………...............

2. TAREHE YA KUZALIWA: ……………………………………………………………………………….................

3. MAHALI ALIPOZALIWA: WILAYA……………………………………MKOA……………………................

4. MAHALI ANAPOISHI KWA SASA: MTAA........................ KATA..........................................

TARAFA: .............................WILAYA: ...........................MKOA.....................................

5. URAIA: MTANZANIA/SIYO MTANZANIA: .......................................KABILA ……………………

6. SHULE NILIYOTOKA: ……………………………………………………………………………………………...........

7. NAMBA YA MTIHANI (CSEE); ……………… SHULE NILIYOFANYIA MTIHANI KIDATO CHA NNE:

……………………………………..WILAYA YA: ………………………………….MKOA: ……………………

**B KUKUBALI NAFASI NA MAELEKEZO ULIYOPEWA**.

MIMI ………………………………………KIDATO CHA…………MWAKA……………..MCHEPUO WA……………
Nimesoma na kuyaelewa maelekezo yote. Hivyo nakubali kuipokea/sikubali kuipokea nafasi niliyopewa. Nathibitisha kwamba nimekubali kujiunga na shule hii kwa hiari na nimepokea maagizo na maelekezo bila kulazimishwa na naahidi kuyazingatia na kutimiza yale ninayopaswa kutimiza bila kulazimishwa. Nitasoma kwa bidii ili nifaulu mitihani yote ya ndani na ya nje.
TAREHE: ……………………………………………………………..SAINI: ………………………………………………

**C. KUKUBALI SHERIA ZA SHULE:**

**MWANAFUNZI**:

Mimi: ………………………………………............................................................................................ nimezisoma na kuzielewa sheria, taratibu, kanuni na miongozo ya shule iliyomo kwenye fomu hii na nitakayosomewa wakati wa Orientation course. Ninaahidi kwamba nitazingatia na kutii masharti, sheria, kanuni, taratibu, miongozo ya shule na maelekezo mengine nitakayopewa na walimu, watumishi wasio walimu na viongozi wote wa shule. Sitashiriki katika mgomo, fujo, wala makosa ya jinai yaliyoorodheshwa hapo juu. Nikivunja au kukiuka maelekezo na sheria yoyote niko tayari kuwajibishwa kulingana na adhabu zilizoorodheshwa kwa kila kosa.

**D. TAARIFA YA MZAZI/MLEZI;(ANDIKA MAJINA MATATU)**

1. JINA LA BABA: ……………………………………………………………MAHALI ANAPOISHI: ………………… YUKO HAI /AMEFARIKI ……………………………KAZI YA BABA: ……………………………………………

SIMU YA BABA………………………………………………………………………………………………………

S.L.P. ……………………MJI…………………………………………………………………………………

2. JINA LA MAMA…………………………………………………………MAHALI ANAPOISHI …………………… YUKO HAI /AMEFARIKI ……………………………KAZI YA MAMA: …………………………………………

SIMU YA MAMA…………………………………………………………………………………………………….

S.L.P. ………………………MJI………………………………………………………………………………

ENDAPO MWANAFUNZI ANALELEWA NA MLEZI:

3. JINA LA MLEZI WA KIUME……………………………………… MAHALI ANAPOISHI……………………

UHUSIANO……………………………………SIMU: ……………………………………………………… JINA LA MLEZI WA KIKE ……………………………………MAHALI ANAPOISHI……………………

UHUSIANO……………………………………SIMU…………………………………………………………

S.L.P. ……………………MJI………………………………………………………………………………

**E. MZAZI/MLEZI (AZAJE SEHEMU HII):**

Mimi…………………………………………………nikiwa Mzazi/Mlezi nimezisoma sheria na maagizo mengine ya shule yanayomhusu mwanafunzi…………………………………………na ninaahidi kutimiza wajibu wangu kama Mzazi/Mlezi wa mtoto huyu kwa: kumshauri ipasavyo ili awe mwanafunzi mwenye nidhamu na ufaulu mzuri.
Pia naahidi kulipa ada ya shule na michango itakayokubaliwa na kumtimizia mahitaji yake ya shule. Nitahudhuria vikao vya shule kwa kadri vitakavyokuwa vinaitishwa na endapo sitahudhuria nitakubaliana na maamuzi yatakayokuwa yametolewa na nitawajibika kulingana na maamuzi hayo.

TAREHE: ……………………………………………………SAINI: ………………………………………………

**F: SEHEMU YA NDUGU WA KARIBU:**

Ndugu wa karibu wanne (4) wanaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi.

MAJINA MATATU MFANO: ROSE JUMANNE MASUMBUKO.

| | JINA | UHUSIANO: | NAMBA ZA SIMU: |
|---|---|---|---|
| | …………………………………………… | …………………………… | ………………………… |
| 1. | …………………………………………… | …………………………… | ………………………… |
| 2. | …………………………………………… | …………………………… | ………………………… |
| 3. | …………………………………………… | …………………………… | ………………………… |

| | | | |
|---|---|---|---|
| PICHA YA NO.1 | PICHA YA NO.2 | PICHA YA NO.3 | PICHA YA NO.4 |

**OORODHA YA VITABU AMBAVYO MZAZI ANAWEZA KUVINUNUA KWA AJILI YA MWANAE KUJISOMEA YEYE BINAFSI.**

**a. Chemistry**

i). Advanced level organic chemistry by APE network 2012
ii). A' level secondary Education chemistry practical iii). Advanced inorganic chemistry volume I and II by S. CHAND iv). Environmental chemistry and pollution control by S. CHAND v). Essential physical chemistry by S. CHAND vi). Selected topics in inorganic chemistry by Wahid U. Malik et al vii). Organic chemistry by S. CHAND

**b. Physics**

i). A' level physics 4th edition. By Roger Muncaster
ii). S. Chand's principle of physics for class xi iii). S. Chand's principle of physics for class xii iv). Nelkon & Parker 7th edn v). University physics vi). Calculation for A' level physics vii). Engineering physics **c.**

**Biology**

i). CJ CLEGG with DG MACKEAN (2000) Advanced Biology principles and Application 2nd Ed,
Hodder Murray London ii). Sylvia S Mader (1996), Biology ( 5th Ed ) Wm C. Brown publisher London iii). DJ Taylor et al (1997), BIOLOGICAL SCIENCE, Cambridge university press – New York.
iv). MBV Roberts (1986), Biology A functional Approach ( 4th Ed )
v). Ann Fullick et al (2011), A level Biology, students Book, Longman. **d.**

**General studies**

i). General studies for A' level certificate form v by. RICHARD R MBALASE
ii). General studies for A' level certificate form vi. By RICHARD R. MBALASE e.

**Geography**

i). Practical geography Alive by Zisti

- Map Reading, photography Interpretation, Field Research, Statistics, and Survey Illustrated by Ellias Anthony Mkoko
- Affordable Edition for secondary and High school learners kot publishers ii). A comprehensive approach to physical geography by D.T. Msabila iii). Human and Economical Geography by Gillan C. Morgan iv). Soil and Climatology by Zisti **f.**

**Mathematics**

i). Pure mathematics 1 by J.K Backhouse
ii). Pure mathematics 2 by J.K Backhouse iii). Pure mathematics 1 L. Bostock and Chandler iv). Advanced mathematics, Tranter CJ


v). S. Chand's mathematics volume 1, Fourth Edition by H.K Dass and RAMA VERMA

vi). S. Chand's mathematics volume 2, Fourth Edition by H.K Dass and RAMA VERMA
vii). Potics in Algebra by DR. P.N.ARORA

**KIWAHILI**

USHAIRI

JINA LA KITABU Kimbunga - H. Goro
Fungate ya uhuru - M.S. Khatibu
Chungu tamu - T.A. Mvungi

RIWAYA

- Vuta nkuwte S.A. shafi
- Usiku utakapokwisha - M. Msokile
- Mfadhili - H. Tuwa

TAMTHILIYA

- Morani - E. Mbogo
- Nguzo mama - P. Muhando

. Kiwli kinaishi St Mohamedi

2.Kiswahili Sakondari - kidato cha V å Vt Oxford,


1. Hallert, R.(1983). Africa Since 1875 Vol. 3. East African Educational Publishers. Nairobi, Kenya.
2. July, R.W. (1992). A History of the African People, East African Educational Publishers, Nairobi, Kenya.
3. Illife, J. (1995). Africans, the History of the Continent . Edinburg, Cambridge; University Press, London UK.
4. Manning, P. (1990). Slavery and African Life; Occidental Oriental and African Slave trade, Cambridge University Press.
5. Njiro, E. (1989). A History of Africa in the 19th century. Literature Bureau Nairobi, Kenya.
6. Rodney, W. (1976). How Eurooe underdeveloped Africa, Publishing House: Dar es salaam, Tanzania.
7. Shillington, K. (2004). History of Africa. MacMillan Publishers. Hong Kong, Japan.

8. Davidson, E. ef al (1997); The growth of the African civilization East and Central Africa to the late 19th century, Longman Group Limited, Singapore.

9. Freud, B. (1998): The making of contemporary Africa; The Development of African societies since 1800, tolorado, Lynne Rienner Publishers.

10. Kimambo, I and Temu, A (1969); A History of Tanzania, East Africa Publishing
Nairobi, Kenya.

11 Robin, H. (1993); African since 1875 A modern History, East African Publishers Ltd., Nairobi, Kenya.

12. Roland, O. and Anthony, A. (2007). Africa since 1800, Cambridge University Press, work, USA.

## READING LIST FOR HISTORY TWO.

1. Nelson throne Essential modern world history
2. History of 21st century (World history) (Oxford)
3. H.L. Peacock. A History of Modern Europe 1789-1981 seventh Edition (2010)
4. The History of Modern World (2007) 6th Edition by Oxford University Press.

### GENERAL STUDIES

1. Richard, R.F. Mbalase. General Studies For Advanced Level Certificate;
2. Mgaywa, B.M. General Studies for Advanced level 3rd Ed.
3. Joannes BigirwaMungu & Sospeter.M. Deogratias. Understanding Advanced Level general Studies;

### GEOGRAPHY DEPARTMENT

1. (colin Buckle), LANDFORMS IN AFRICA
2. C.R. KOTHARI), RESEARCH METHODOLOGY
3. (H.c. TRURAN), A PRACTICAL GUIDE TO STATISTICAL MAPS AND DIAGRAMS
4. (Goh Cheng Leong.Gillian.C. Morgan), HUMAN AND ECONOMIC GEOGRAPHY
5. (DAVID WAUGH), GEOGRAPHY-AN INTIGRATED APPROACH.

**SHERIA NA KANUNI ZA SHULE YA SEKONDARI MAZAE**

Shule ya Sekondari Mazae inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 pamoja na marekebisho yake. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Kijana anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na kupewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a. Heshima kwa viongozi, wazazi/walezi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa jumla ni jambo la lazima.
b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za ndani na nje ya shule ni muhimu na lazima.
c. Kutimiza kwa makini maandalizi ya jioni(Night Preparation)
d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyinginezo utakazopewa.
e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f. Kutunza usafi wa mwili pamoja na mazingira ya shule kwa jumla.
g. Kuvaa vizuri huku ukiwa umechomekea sare ya shule wakati wote.
h. Kuzingatia ratiba yote ya shule wakati wote kuanzia asubuhi wakati wa kuamka hadi usiku wakati wa kwenda kulala.
i. Mwanafunzi haruhusiwi kuvuta sigara, kufuga kucha na nywele ndefu wala kusuka.
j. Ni lazima mwanafunzi aheshimu na kukubali tofauti za ki dini, ki utamaduni na siasa zilizomo katika jumuiya yetu.

***Tafadhali sana katika kumleta au kumsafirisha kijana wako zingatia sana siku na muda wa kazi. (Siku za Jumamosi, Jumapili na Sikukuu za Kitaifa siyo siku za kazi)***

**Hongera na Karibu Sana Shule ya Sekondari Mazae**

**……………………………**
**Shangaluka G.C**
**MKUU WA SHULE**